# Tanzania

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Mkuu wa Nchi na Serikali: **John Pombe Magufuli**

**Serikali iliminya haki za uhuru wa kujieleza, kujumuika na kukusanyika kwa amani wakati wa kuelekea chaguzi za mwezi Oktoba. Mnamo mwezi Juni, Rais aliitangaza Tanzania kutokuwa na maambukizi ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO-19). Mamlaka zilizuia uhuru wa vyombo vya habari, zikidai kuwa zilikuwa zikizuia "kuenea kwa taarifa za uongo" kuhusu janga la ugonjwa huo. Vyombo vya habari vilifungwa kwa kutoa taarifa kuhusu matukio ya kisiasa. Wanafunzi wajawazito walizuiwa kuendelea na shule na kutengwa kwa kupelekwa kwenye vituo vya elimu mbadala.**

## Usuli

Tarehe 28 Oktoba, Tanzania ilifanya uchaguzi wake mkuu kwa mara ya sita tangu kuanzishwa tena kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992. Mnamo mwezi Novemba, Rais alianza muhula wake wa pili madarakani kufuatia uchaguzi wenye utata. Katika kuelekea uchaguzi, wakati na baada ya uchaguzi, wanasiasa wa upinzani na mamia ya wafuasi wao walikamatwa kiholela na kupigwa na polisi, na wengine waliuawa. Wanasiasa kadhaa, akiwemo Tundu Lissu, mgombea wa urais kupitia chama cha Chadema, chama kikuu cha upinzani, na mwanasiasa wa upinzani, Lazaro Nyalandu na Godbless Lema na familia yake walikimbia nchi baada ya uchaguzi, kwa kuhofia kuteswa.

## Haki ya Afya

Serikali ilizuia taarifa zinazohusiana na UVIKO-19 na kupuuza mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kuhusu namna gani serikali, wataalamu wa afya na umma kwa jumla wanapaswa kulishughulikia janga hilo la ugonjwa. Hakukuwa na mfumo unaoaminika au wa haraka wa kutoa taarifa sahihi juu ya ugonjwa huo mwishoni mwa mwaka. Mnamo 29 Aprili, serikali iliacha kuchapisha taarifa kuhusiana na viwango vya maambukizi. Tarehe 5 Juni, Rais aliitangaza nchi kutokuwa na maambukizi ya UVIKO-19 jambo ambalo liliwawia vigumu Watanzania kuchukua hatua za kutosha za kujikinga na maambukizi.

### Hali za magereza

Mnamo mwezi Aprili, Rais aliwasamehe wafungwa 3,717 kwa kuzingatia mapendekezo ya WHO ya kupunguza wingi wa wafungwa kwenye magereza ili kuzuia maambukizi ya UVIKO-19. Hata hivyo, magereza yaliendelea kuwa na idadi kubwa sana ya wafungwa, hali iliyoweka hatarini afya ya wafungwa. Kulikuwa na wafungwa 32,438, ambapo kati yao, wafungwa 17,974 walikuwa rumande; idadi ya wafungwa ilikuwa 9% zaidi ya nafasi kwenye magereza.

## Ubaguzi - wanawake na wasichana

Wasichana wajawazito na akina mama wenye umri mdogo walibaguliwa katika sekta ya elimu. Serikali iliendelea kuwazuia kuendelea na shule na ilitumia mkopo wa Benki ya Dunia - uliolenga kuboresha elimu ya sekondari kwa wasichana - kuendeleza ubaguzi wao katika vituo vya mafunzo mbadala, ambapo mtalaa wa miaka minne wa elimu ya sekondari ya kawaida ulipunguzwa na kuwa wa miaka miwili.

## Ukandamizaji wa upinzani wa mawazo

Mamlaka zilitumia sheria kunyamazisha upinzani wa mawazo wa amani na kuzuia sana haki ya uhuru wa kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari, hususan katika kipindi cha kuelekea uchaguzi.

Mnamo mwezi Aprili, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoza vyombo vya habari vya *Star Media Tanzania limited*, *Multichoice Tanzania Limited* na *Azam Digital Broadcast Limited* faini ya shilingi za kitanzania milioni 5 (dola za kimarekani 2,150), na kuamuru vyombo hivyo kuomba msamaha kwa "kueneza taarifa za uongo na za kupotosha" juu ya namna serikali inavyokabiliana na janga la UVIKO-19, kosa ambalo ni kinyume na Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania. Baadaye katika mwezi huo huo, TCRA ililisimamisha *Mwananchi,* gazeti la mtandaoni, kwa miaka sita na kulipiga faini ya shilingi za kitanzania milioni 5 (dola za kimarekani 2,150) kwa kuchapisha picha ya Rais ambayo ilimuonesha akikiuka miongozo ya kukaa mbali mbali baina ya mtu na mtu. Mamlaka ilisema kuwa *Mwananchi* ilikuwa imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Kimtandao) za mwaka 2018.

Serikali ilitoa adhabu kwa magazeti na vituo vya utangazaji, hususan kati ya mwezi Juni na Oktoba, kwa kuripoti matukio ya kisiasa yanayohusiana na uchaguzi. Gazeti la *Tanzania Daima* lilipewa katazo lisilo na muda kwenye machapisho yote na usambazaji; televisheni ya mtandaoni, *Kwanza TV*, ilifungiwa kwa miezi 11, na *Clouds TV* na *Clouds FM Radio* zilifungiwa kwa siku saba.

Mnamo mwezi Agosti, TCRA ilirekebisha Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) kuzuia vyombo vya habari vya kimataifa kutoa taarifa kuhusu uchaguzi. Vyombo vya habari vya ndani vililazimika kupata ruhusa ya mdhibiti ili kurusha matangazo yanayotolewa na, au kwa ushirikiano na vyombo vya habari vya nje. Marekebisho hayo pia yaliwataka waandishi wa habari wa nje kusindikizwa na viongozi wa serikali wanapokuwa wanafanya kazi zao.

## Watetezi wa haki za binadamu

Mamlaka ziliwaweka watetezi wa haki za binadamu katika hali ya kuwa na hofu, kufanyiwa usumbufu, vitisho, kukamatwa kiholela na kuwekwa kizuizini, na kufunguliwa mashtaka. Mashirika ya haki za binadamu yalifungwa au kusimamishwa iwapo hayakutimiza masharti mengi yaliyotolewa na sheria na kanuni mbalimbali.

Mwanasheria wa haki za binadamu Tito Elia Magoti na Theodory Giyani walibaki kizuizini kufuatia kukamatwa kwao kiholela mnamo mwezi Disemba 2019. Walikamatwa kutokana na shughuli zao kwenye mtandao wa kijamii na kushtakiwa chini ya sheria mbalimbali, ikiwemo Sheria ya Makosa ya Mtandao, kwa "kumiliki programu ya Kompyuta iliyobuniwa kwa lengo la kufanya uhalifu", pamoja na "kujihusisha na genge la uhalifu na utakatishaji fedha". Kesi zao ziliahirishwa zaidi ya mara 10 na mahakama iliyopo jijini Dar es Salaam baada ya upande wa mashtaka kuomba mara kwa mara muda zaidi wa kumalizia uchunguzi wao.

Mnamo mwezi Julai, polisi ilimkamata Sheikh Issa Ponda, kiongozi wa dini ya Kiislamu, wa wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam. Polisi walimshikilia kwa siku 10 kwa kusambaza makala ambayo walidai ilipelekea uchochezi na kuvunjika kwa amani wakati wa kuelekea uchaguzi. Katika makala yake, alionesha umuhimu wa kuwepo kwa chombo huru cha uchaguzi na alikuwa amedai kuwa waislamu walikabiliwa na ubaguzi, hususan katika ajira za serikali. Baada ya kuachiwa kwake, watu alioamini kuwa polisi walimtishia kumkamata tena na mwezi Agosti alienda mafichoni, ambako alikaa hadi mwisho wa mwaka.

## Uhuru wa kujumuika

Serikali iliendelea kudhibiti na kuzuia kazi ya mashiririka yasiyo ya kiserikali (NGOs), ikiminya sana haki ya uhuru wa kujumuika.

Mnamo 24 Juni, Msajili wa mashirika yasiyo ya kiserikali alisimamisha shughuli za shirika la *Inclusive Development for Citizens*-Tanzania, linalolenga kukuza utawala bora. Shirika hilo lilituhumiwa kwa kushindwa kutoa taarifa za shughuli zake za mwaka 2019, orodha ya wafanyakazi wake na mikataba ambayo shirika hilo lilisaini na wafadhili, pamoja na mambo mengine, jambo ambalo ni ukiukwaji wa Sheria ya Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Kanuni za mashirika yasiyo ya kiserikali.

Siku hiyo hiyo, Msajili alitoa notisi kwa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), akizitaka kujieleza ndani ya siku saba kwa nini hatua za kisheria, ikiwemo ya kufutiwa usajili kwa kutotii sheria za mashirika yasiyo ya kiserikali, zisichukuliwe dhidi ya mashirika hayo. Msajili pia aliiamuru LHRC kusimamisha shughuli zozote zinazohusiana na uchaguzi. Kwa sababu hii, Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilikataa maombi ya mashirika yote mawili ya kuangalia uchaguzi mkuu.

Mnamo mwezi Agosti, THRDC, iliyojumuisha zaidi ya watu na mashirika, ilitangaza kusimamishwa kwa muda kwa shughuli zake baada ya polisi kuamuru kufungiwa akaunti zake kwa kutotii Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. THRDC ilituhumiwa kwa kuingia mkataba na wafadhili bila kuihusisha Ofisi ya Msajili wa Hazina na Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

## Kukamatwa kiholela na kuwekwa kizuizini

Mwezi Juni, katika mkoa wa Kilwa, polisi walimkamata Zitto Kabwe, kiongozi wa chama cha upinzani cha ACT-Wazalendo, pamoja na wanachama wengine saba. Chama kilisema kuwa watu hao walikamatwa kwa tuhuma za "kuhatarisha amani" wakati wakiwa kwenye mkutano ambao polisi walisema ulikuwa kinyume na sheria. Watu hao waliachiwa kwa dhamana siku iliyofuatia na hawakupewa maelezo yoyote kuhusiana na yaliyodaiwa kuwa makosa yao.

Mnamo mwezi Julai, polisi walimkamata Nusrat Hanje, Katibu Mkuu wa Baraza la Vijana Chadema, na wanachama wengine watano, katika mkoa wa Singida magharibi mwa mji wa Dodoma, baada ya kupandisha bendera ya chama huku wakiimba wimbo wa taifa. Mashtaka dhidi yao yalijumuisha "mkusanyiko usio halali, kudharau bendera na wimbo wa taifa, na vitendo ambavyo vingeweza kusababisha uvunjifu wa amani." Watu hao walinyimwa dhamana na kuwekwa kizuizini katika gereza la Singida tarehe 10 Julai ambapo walishikiliwa kwa siku 133, licha ya Mahakama Kuu mjini Dodoma kupitisha rufaa yao dhidi ya kunyimwa dhamana mnamo tarehe 26 Agosti. Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma alifuta mashtaka dhidi ya watu hao sita mnamo tarehe 23 Novemba.

Mnamo mwezi Agosti, polisi walimkamata Joseph Mbilinyi, ambaye alikuwa akigombea ubunge wa jimbo la Mbeya Mjini na kumshutumu kwa kufanya maandamano yasiyo na kibali. Mbilinyi alikamatwa akiwa anaelekea ofisi za mkoa za NEC kuchukua fomu za uteuzi. Aliachiliwa siku hiyo hiyo bila ya kufunguliwa mashtaka.

Mnamo mwezi Novemba polisi walimkamata na kumshitaki Freeman Mbowe, mwenyekiti wa Chadema na wanachama watatu wa chama hicho kwa "makosa ya ugaidi" kwa kuhamasisha maandamano ya nchi nzima ya kupinga mwenendo wa uchaguzi wa Oktoba. Tundu Lissu (Tazama hapo juu, usuli) alikamatwa siku iliyofuatia. Wote waliachiwa kwa dhamana.

## Kutoshtakiwa kwa haki

Mnamo mwezi Februari, Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Dar es Salaam, iliyopo Kisutu ilimuachia mwandishi Erick Kabendera kutoka gerezani baada ya kuingia makubaliano na upande wa mashtaka. Alikuwa ametekwa na watu wasiojulikana mwezi Julai 2019. Saa ishirini na nne baadaye, polisi walithibitisha kuwa alikuwa chini ya ulinzi wao. Baadaye, alishtakiwa kwa utakatishaji fedha na kujihusisha katika genge la uhalifu.

Erick Kabendera alikabiliwa na kesi mahakamani iliyotumia muda mrefu, kesi ambayo iliahirishwa mara 16. Kabendera alisema aliteswa katika gereza la Segerea mjini Dar es Salaam. Pia alisumbuliwa na maradhi ya mara kwa mara na kunyimwa ruhusa ya kwenda kumtembelea mama yake aliyekuwa mgonjwa ambaye alifariki wakati Kabendera akiwa gerezani. Mahakama ilimuamuru kulipa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka ya Umma kiasi cha zaidi ya shilingi za kitanzania milioni 273 (dola za kimarekani 116,000) kwa ajili ya kulipia, pamoja na mambo mengine, linalodaiwa kuwa deni la ukwepaji kodi na faini. Kabendera alitakiwa kulipa madeni hayo ndani ya kipindi cha miezi sita au kukamatwa tena.

Mnamo mwezi Mei, polisi walimkamata mchekeshaji Idris Sultan, na kumuachia baada ya siku 10, kwa dhamana ya shilingi za kitanzania milioni 15 (dola za kimarekani 6,550). Idris alikamatwa kwa kuhusishwa na video aliyoisambaza kwenye mtandao wa kijamii ambako inadaiwa alimdhihaki Rais. Alishtakiwa kwa "kushindwa kusajili laini ya simu ambayo awali ilikuwa ikimilikiwa na mtu mwingine", na "kushindwa kuripoti mabadiliko ya umiliki wa laini ya simu". Kesi yake iliahirishwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Dar es Salaam iliyopo Kisutu kwa angalau mara tisa na kusubiriwa hadi mwisho wa mwaka.

## Haki ya ukweli, haki na fidia

Mnamo mwezi Juni, Bunge lilipitisha Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 3 ya mwaka 2020 ambayo, pamoja na mambo mengine, iliwataka walalamikaji chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu wa Msingi, kuwasilisha hati zinazoonesha kuwa ukiukwaji ulikuwa umewaathiri moja kwa moja. Hivyo, jambo hilo lilidhoofisha madai ya maslahi ya umma na uwajibikaji wa serikali kwa ukiukwaji wa haki za binadamu.